# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz


## UTEKAJI MPAKA LINI?

### Utangulizi

**"Suala la utekaji mpaka lini?"** Ni swali linaloulizwa na wadau wengi wa haki za binadamu, wanasiasa, na wananchi wa kawaida, lakini huenda lisipate jibu la moja kwa moja. Tukitazama historia ya nchi yetu, neno *utekaji* halikuwa msamiati uliokuwa ukitumika sana katika miaka ya awali ya uongozi wa Taifa letu.

### Utekaji katika historia ya Tanzania

Katika awamu ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na awamu ya pili chini ya hayati Ally Hassan Mwinyi, matukio ya watu kutekwa hayakuwa yakiripotiwa. Kwa wakati huo, mazingira ya kijamii na teknolojia duni hasa ukosefu wa mitandao ya kijamii huenda vilichangia ukimya huo. Badala ya neno *utekaji*, Watanzania walizoea msamiati wa *uwekaji kizuizini*, uliokuwa ukitumika kwa mujibu wa amri ya Rais chini ya Sheria ya Uwekaji Watu Kizuizini. Miongoni mwa waliowahi kuwa wahanga wa sheria hiyo ni pamoja na Balozi Christopher Kasanga Tumbo na wengine maarufu.

### Dalili za kwanza za matukio ya kutekwa

Dalili za kwanza za matukio ya kutekwa zilianza kuonekana katika awamu ya nne chini ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Mifano ni tukio la kutekwa kwa Dkt. Steven Ulimboka mwaka 2012 na kupatikana katika msitu wa Mabwepande akiwa ameumizwa vibaya na watu wasiojulikana; kuvamiwa kwa Dkt. Sengondo Mvungi, aliyekuwa mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, na kufariki dunia baadaye nchini Afrika Kusini; kutekwa na kuumizwa kwa Absalom Kibanda, aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF); kumwagiwa tindikali kwa Saed Kubenea, Mkurugenzi wa gazeti la *Mwanahalisi*; na kuuawa kwa risasi kwa Profesa Jwani Mwaikusa tarehe 14 Julai 2010 kwa kutaja kwa uchache. Hata hivyo, licha ya matukio haya, neno *utekaji* halikushika kasi kubwa katika vinywa vya Watanzania.

### Wimbi jipya la utekaji na kudhuru baada ya mwaka 2016

Kuanzia mwaka 2016, matukio ya watu kutekwa na kupotea yaliongezeka kwa kasi. Watu kama Ben Saanane na Azory Gwanda walitoweka katika mazingira ya kutatanisha hadi leo, takribani miaka tisa baadaye, hawajapatikana. Hapo


**Board of Directors:**
Justice (Ret'd) Dr. Fauz A. Twaib- Chairperson, Ms. Josephine A. Zimba- Vice Chairperson, Dr. Anna Henga (Adv.) Secretary, Ms. Anabahati Mlay- Member, Ms. Hellen Kilontsi – Member, Dr. Ringo Tenga – Member, Dr. Ally Laay - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki - Member

ndipo misemo kama *utekaji* na *watu wasiojulikana* ilipoanza kuzoeleka miongoni mwa Watanzania. Kushambuliwa hadharani kwa mwanasiasa Mh. Tundu Lissu ni tukio lingine la kusikitisha ambalo hadi leo hakuna majibu ni nani alihusika na hakuna taarifa yoyote iliyowahi kutolewa hadharani juu ya upelelezi wa tukio hili.

**Sababu na dhana zinazotajwa**

Zipo dhana kuu mbili kuhusu matukio haya ya utekaji. Kwanza, yapo matukio yaliyothibitishwa na Jeshi la Polisi. Pili, yapo matukio yaliyoripotiwa na familia za wahanga lakini yasiyothibitishwa na vyombo vya dola. Sababu zinazotajwa ni nyingi: kisiasa, wivu wa mapenzi, imani za kishirikina, visasi, au misimamo mikali ya kiitikadi.

**Katiba na utawala wa sheria**

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ibara ya 13(6)(a)(b), 107A(1), 3, na 4, Tanzania ni nchi inayofuata utawala wa sheria. Chombo pekee chenye mamlaka ya kutoa adhabu au kuamua hatima ya mtu ni mahakama. Ibara ya 59B na Sheria ya Ofisi ya Mashitaka ya Umma (Sura ya 430, toleo la 2023) zinatoa utaratibu wa kisheria wa kushughulikia tuhuma. Kwa lugha rahisi, hakuna chombo kingine kinachopaswa kutoa adhabu nje ya mfumo wa mahakama.

**Juhudi za familia na wadau wa haki**

Licha ya wito wa kuheshimu na kulinda haki, juhudi za familia nyingi zimegonga mwamba. Wengi wamekwenda  katika ofisi za makamanda wa polisi wa mikoa, makao makuu ya Jeshi la Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani, na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora bila mafanikio. Mfano ni kesi za Deus Soka, Jacob Mlay, Frank Mbise na Mdude Nyagali (Nyagali Mpaluka), ambapo maombi ya *Habeas Corpus* yaliwasilishwa mahakamani lakini hayakuzalisha matokeo. Hata maagizo ya mahakama kwa jeshi la polisi kufanya uchunguzi wa kina hayajatekelezwa.

Kwa sasa, maombi kama hayo yapo tena mahakamani kufuatia madai ya kutekwa kwa Ndugu Humphrey Polepole, kada wa CCM na aliyewahi kuwa Mbunge wa kuteuliwa, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, na Balozi wa Tanzania nchini Cuba na Malawi. Hili limeibua mjadala mkubwa: kama mtu wa ngazi hiyo anaweza kutekwa bila hatua za haraka, hali ya wananchi wa kawaida ikoje?

**Board of Directors:**
**Justice (Ret'd) Dr. Fauz A. Twaib- Chairperson, Ms. Josephine A. Zimba- Vice Chairperson, Dr. Anna Henga (Adv.) Secretary, Ms. Anabahati Mlay- Member, Ms. Hellen Kilontsi – Member, Dr. Ringo Tenga – Member, Dr. Ally Laay - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki - Member**

**Wahanga wapya na maswali mapya**
Wakati mwanzoni wimbi hili lilionekana kulenga aina fulani za watu maswali mapya yanaibuka hasa kwa matukio mapya ya Daniel Nchonchorio- Mjumbe wa Mkutano mkuu CCM Mwanza aliyetoweka huko Mwanza na hadi leo hakuna majibu pamoja na Siza Kaheta aliyekuwa Mtia nia CCM udiwani kata ya Ganyange Tarime vijijini.

**Taarifa ya Jeshi la Polisi na mashaka ya umma**
Baada ya Baraza Kuu la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kuishutumu Tanzania kuhusu vitendo vya utekaji, Jeshi la Polisi lilitoa taarifa tarehe 18 Juni 2025 kupitia msemaji wake DCP David Misime, likitoa takwimu na sababu za baadhi ya matukio. Hata hivyo, taarifa hiyo ilikosolewa umma kwa kuangazia zaidi matukio ya wivu wa mapenzi, visasi, na imani za kishirikina, huku ikinyamazia matukio yenye taswira za kisiasa. Taarifa ya polisi ilishindwa kujibu mambo ya msingi mfano kutekwa na kuuliwa kwa Ally Kibao, kutekwa na kuumizwa kwa Edger Mwakabela(Sativa).

**Maswali yanayojitokeza**
Watanzania wengi sasa wanajiuliza: watu wasiojulikana ni akina nani? Watendelea kutojulikana mpaka lini? Wanafanya haya kwa masilahi ya nani? Utekaji hauna afya kwa Taifa letu. Unaleta hofu, unaharibu taswira ya nchi kimataifa, na unaondoa imani ya wananchi kwa vyombo vya dola.

**Chanzo cha tatizo: Sheria za Haki Jinai zenye mianya**
Tangu Tume ya Jaji Nyalali (1993) na baadaye Tume ya Haki Jinai ya Jaji Othman Chande (2022), mapendekezo ya kufutwa kwa Sheria ya Uwekaji Watu Kizuizini bado hayajatekelezwa. Huenda mijadala ya umma na malalamiko mengi kuhusu utekaji yanatokana na mianya iliyopo kwenye sheria zetu hasa za jinai ambazo zinatoa mamlaka kwa baadhi ya taasisi kuweka watu kizuizini bila maelezo ya kina au kukamata watu bila kufuata utaratibu wa kisheria.

**Hitimisho**
Ni wakati sasa, kama Taifa, tuseme kwa pamoja: basi! Vitendo vya utekaji vinapaswa kukomeshwa mara moja. Utekelezaji wa sheria, uwazi wa vyombo vya dola, na heshima kwa haki za binadamu ni nguzo za amani na ustawi wa Taifa letu.

**Imetolewa na:**
***Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)***
**Tarehe: 13 Oktoba 2025**

**Board of Directors:**
Justice (Ret'd) Dr. Fauz A. Twaib- Chairperson, Ms. Josephine A. Zimba- Vice Chairperson, Dr. Anna Henga (Adv.) Secretary, Ms. Anabahati Mlay- Member, Ms. Hellen Kilontsi – Member, Dr. Ringo Tenga – Member, Dr. Ally Laay - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki - Member